بسم الله الرّحمن الرحيم

18/Safar/1427H=18/March/2006Ad,Madinatul Rassuuli llahi {s.a.w}
- Saudi Arabia.makala namba 2.

HII NDIYO DAAWA YETU

JUU YA UFAHAMU WA SALAF SWALIHI

# ATHARI MBAYA YA UZUSHI KATIKA UISLAMU.

*amesema swahaba mtukufu Abdullahi ibin Umar ibin al khattabi{r.a.};*

**كل بدعة ضلالة وإن رآها الناس حسنا**

*[Bidaa zote ni upotevu hata kama watu wataziona kuwa ni nzuri].*

*Ameitaja athari hii Imamu al Bayhaqy katika kitabu chake al mad'khal ukurasa 191,na Imamu al Laalakai katika kitabu chake shar'hu usuulil i'tiqadi ukurasa126.*

MUANDISHI;

AL AKH QASSIM MAFUTA QASSIM.

بسم الله الرّحمن الرحيم

Ewe mola wetu ni zako wewe sifa njema zote,na shukrani zote.
Ni zako wewe sifa njema vile zinavyo lingana na utukufu wako,na ukubwa wako,ni zako wewe sifa njema mpaka uridhike,na pale unaporidhika, na baada ya kuridhika.

Na sala na salamu zimfikie kipenzi chetu,Mtume wetu Muhammad, na jamaa zake,na maswahaba zake wote,na walioiandama njia yao kwa wema mpaka siku ya malipo.

Katika makala hii namba mbili tutazungumzia juu ya baadhi hoja zao ambazo wanazitegemea

Ndugu zetu hawa watetezi wa maulidi, wana hoja zao nyonge sana,lakini

wenyewe wanaziona ni hoja zenye nguvu,kwahoja hizo hawako tayari kuwacha uzushi wao huo,na hoja zao hizo zimegawanyika katika sehemu kuu mbili;

a)kuna hoja zinazoonekana kuwa ni za kielimu.

b) kuna zile hoja zisizo za kielimu -nazo ndio nyingi- na asili ya hoja hizo kutoka kwa watu wasio soma kisha waliosoma nao huwafuata wafuasi wao katika kuzitumia hoja hizo,kuishiria namna walivyo filisika kihoja !

Sisi-In'shaallah- tutazijibu zile ambazo kidogo zinawatatiza watu hasa ambao hawakusoma,au wanaupeo mdogo wa kielimu,na wanapenda kujua haki na ukweli ili waufuate,
hebu sasa tuanze uchambuzi wa hoja hizo kwa idhini ya Allah{s.w.t.};

## HOJA ZAO ZA KUHALALISHA UZUSHI KATIKA DINI.

**Hoja yao ya kwanza;**

Siyo kila ambalo hakulifanya Mtume {s.a.w.} ni bidaa na ni upotevu,bali jambo litaangaliwa kama ni baya halito kubaliwa,na kama ni zuri litakubaliwa.

kwasababu Bwana Mtume{s.a.w.} amesema;

"من سن فى الاسلام سنة حسنة فله أجره..."

[Mwenye kuanzisha katika uislamu sunna nzuri atapata ujira wake…].

Na sisi tunaitakidi kwamba watu kukusanyika na kusoma maulidi ni jambo zuri hata kama mtume{s.a.w. } hakufanya,na katika hadithi hii limetumika neno Sanna lenye maana ya kuanzisha na siyo kuhuisha kama mnavyo tafsiri nyinyi mawahabi..!

**Jawabu yake ni kama ifuatavyo;**

1-Hadithi hii haitumiki katika mambo ambayo hayakufundishwa katika dini,bali inatumika katika mambo ambayo yamefundishwa kisha watu wakayawacha ima kwa kukusudia au kwa kusahau kwasababu zifuatazo;

(a)Sababu ya Bwana Mtume {s.a.w.} kusema maneno haya Bwana Mtume {s.a.w.} alisema maneno haya kwa munasaba maalumu,-yaani kuna sababu wurudil hadithi-kama wanavyo tueleza wataalamu wa mambo ya hadithi.

Swahaba Jarir bin Abdillahi{r.a.} anasimulia kwa kusema;

[siku moja tulikuwa kwa Mtume{s.a.w.} mwanzoni mwa mchana wakaja watu wakiwa wamevaa shuka za sufi, na hali ya kuwa wamezichomoa panga zao,na wote ni watu wa kabila la mudhari,ghafla ukabadilika uso wa Mtume{s.a.w.} -kwa huzuni-

kutokana na alivyo ziona hali zao za ufakiri,akaingia ndani{s.a.w.} kisha akatoka, kisha akamuamrisha Bilali - aadhini na akimu Swala- Bilali akaadhini kisha akakimu,na Mtume{s.a.w.} akaswali,kisha akawahutubia watu akasema;

[Enyi watu nyie! muogopeni mola wenu ambaye amekuumbeni kutokana na nafsi moja…mpaka mwisho wa hotuba yake- iliyokuwa inahamasisha kutoa.

lakini watu hawakutoa- ndipo kaja Bwana mmoja katika Answaari ( wa Madina) na mrundo ambao mkono wake ulishindwa kuubeba,
akasema Jarir{r.a.}-baada ya kuanza kutoa Answaari huyo);

watu walifuatia -kutoa- mpaka nikaiona mirundo miwili ,mrundo wa chakula na mrundo wa nguo, nikauona uso wa Mtume{s.a.w.} una meremeta kama fedha iliyo nyunyiziwa dhahabu,

kisha akasema(Bwana Mtume s.a.w.);

[mwenye kuhuisha katika uislamu sunna nzuri atapata ujira wake na ujira wa wale watakaoifanya sunna hiyo baada yake…].

Hiyo ndiyo sababu na mnasaba wa Bwana Mtume{s.a.w.} kusema maneno haya.

Sasa Kama neno sanna hapa lina maana ya kuzusha jambo jipya ambalo halikufundishwa na uislamu.

Je ni lipi jipya alilo lizusha Answari huyu ambalo halikufundishwa katika uislamu?

Je ni huko kutoa? Mbona kutoa kulikuweko tangu Mtume{s.a.w.} yuko Makka? kwani ninani aliye mnunua Sayyid'na Bilali?

Hebu isome aya ya 17-21 ya suratul layli(92).

Je nikinani walio mkirimu Mtume{s.a.w.} na maswahaba zake pindi walipofika Madina?

(b)Bwana Mtume{s.a.w.} amesema; [ mwenye kuanzisha SUNNA NZURI] - kama wanavyo tafsiri wao- na hakusema;[ mwenye kuzusha BIDAA NZURI].

Na sote tunakubaliana kwamba bidaa siyo sunna,na sunna siyo bidaa,kwasababu hakuna bidaa nzuri katika sheria,bali kila bidaa katika dini  ni upotevu na upotevu wote ni motoni,ama madai ya baadhi ya wanawachuoni kwamba eti kuna bidaa nzuri katika dini madai hayo siyo sahihi.

Amesema swahaba mtukufu Abdullahi ibin Umar ibin al khattabi{r.a.};

**كل بدعة ضلالة وان رآها الناس حسنا**

**[Bidaa zote ni upotevu hata kama watu wataziona kuwa ni nzuri].**

Hayo ni maneno ya swahaba wa Mtume{s.a.w.} kwamba hakuna katika uislamu bidaa iliyonzuri.Ameitaja athari hii Imamu al Bayhaqy katika kitabu chake al mad'khal
ukurasa 191,na Imamu al Laalakai katika kitabu chake shar'hu usuulil i'tiqadi ukurasa126.

Na amesema Imamu Maalik{r.a.};

**فقد زعم أن من ابتدع فى الاسلام بدعة يراها حسنة)**
**لأن الله يقول,محمدا خان الرسالة:**
**{ الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَ تِي**
**وَرَضِيتُ لَكُمُ الإِسْلاَمَ دِيناً .. }**
**المائدة3**
**فما لم يكن يومئذ دينا فلا يكون اليوم دينا**

[mwenye kuzusha katika uislamu bidaa akiona kuwa ni nzuri,basi atakuwa amedai kwamba Muhammad{s.a.w.} amefanya hiyana katika (kufikisha)

ujumbe,kwasababu amesema
Allah{s.w.t.};

"leo nimekukamilishieni Dini yenu,na
nimekutimizieni neema yangu,na
nimeuridhia kwenu uislamu kuwa ndiyo
Dini.." al maidah 3,
basi lile ambalo halikuwa dini siku hizo
haliwezi likawa ni dini hii leo].
Tazama kitabu al i'tiswaam 1/49.

Na hayo ni maneno ya Imamu mkubwa
katika Maimamu wanne wa Ah'lis Sunna,
basi yazingatie.

Lakini jambo kubwa la kushangaza kwa
ndugu zetu hawa watetezi wa mambo ya
uzushi ni pale wanaposema;

tunakubali kwamba haya maulidi ni bidaa,lakini ni bidaa nzuri!!
Na bila shaka umemuelewa Imamu Malik kwamba atakaye zusha bidaa katika dini kisha akadai kuwa ni bidaa nzuri,
basi atakuwa ameshamtuhumu Bwana Mtume {s.a.w.} katika ufikishaji wake!

Halafu lakushangaza zaidi ni pale wanapotakiwa kutoa dalili ya kufaa hiyo bidaa nzuri-kama wanavyodai - ghafla utawaona wanaitumia hadithi hii inayosema;

**"mwenye kuhuisha katika uislamu sunna nzuri…!"**

hivi kweli hawajui tafauti ya sunna na bidaa?! Au wanakusudia kuwababaisha watu kama kawaida yao?

(c)na ama kuhusu neno sanna katika hadithi hii lina maana ya kuhuisha na siyo kuanzisha,amesema Imamu Ashaatwiby

kwenye kitabu chake al Itiswaam juzuu 1 ukurasa 182;

ليس المراد:
الاستنان بمعنى الاختراع,

وانما المراد به العمل بما ثبت بالسنة النبوية

وذلك لوجهين:
:
أحدهما
أن سبب الذي جاء لأجله الحديث هو الصدقة :
المشروعة...."

"Si makusudio ya (neno) sanna kwa maana ya kuzusha,hakika makusudio yake ni kufanya lile ambalo limethibiti katika sunna ya Mtume{s.a.w},na hilo kwasababu mbili;

moja kati ya hizo; ni kwamba sababu ambayo Hadithi imekuja kwa ajili yake ni sadaka ambayo iko katika sheria….”.

pengine mtu anaweza kuhoji; ikiwa katika uislamu kuna sunna nzuri, je sunna mbaya nizipi?

Au kwa ibara nyingine je kuna sunna mbaya?

Jawabu ndiyo!

Ziko suna mbaya, nazo ni yale mambo ya maasia ambayo  sheria imeyaharamisha.

## Hoja yao ya pili;

Siyo kila ambalo halikufanywa na Mtume{s.a.w.} halifai kulifanya,na kama kila ambalo hakulifanya mtume{s.a.w.} halifai, na ni uzushi,mbona Umar{r.a.} amezusha swala ya tarawehe?

Tena akasema wazi kuwa;"نعمت البدعة هذه"
[bora ya uzushi ni huu]?
Je hamuoni kwamba yafaa kuzusha? na kuwa kuna uzushi mwingine katika dini ni mzuri?

**Jawabu yetu ni kwa njia tatu;**

1- kama tulivyotangulia kusema kwamba,jambo lolote lile ambalo Mtume{s.a.w.} hakulifanya,
na sababu za kulifanya jambo hilo zilikuweko,na hakukuwa na kizuizi chochote cha kumzuia,basi kulifanya jambo hilo ni uzushi,
na siyo kweli kusema kwamba Umar{r.a.} ndiye aliyezusha swala ya tarawehe,bali swala ya tarawehe aliye ianzisha ni Bwana Mtume{s.a.w.} kama ilivyothibiti kwa maandiko sahihi.

Amepokea Imamu Bukhary,na Imamu Muslimu katika sahihi zao,kutoka kwa Bi Aisha mke wa Mtume{s.a.w.} amesema;

“Ameswali mtume wa mwenyezi mungu{s.a.w.} msikitini katika usiku mmoja,wakaswali watu-nyuma ya- swala yake,
kisha akaswali usiku uliofuatia watu wakawa wengi,kisha wakakusanyika katika usiku wa tatu akatoka{s.a.w} akaswali na watu wakaswali nyuma yake,ulipofika usiku wanne Mtume{s.a.w.}hakutoka,kulipo pambazuka asubuhi,
akasema Mtume{s.a.w.}; nimewaona mlivyofanya(mlivyokusanyika) hakuna jambo lililo nizuia kutoka isipokuwa ni kuogopea isije ikafaradhishwa juu yenu”.

Tazama sahihi Bukhary Hadithi namba 1129,na sahihi Muslimu Hadithi namba 761.

-Kwa hivyo basi,kauli ya kusema kwamba Umar{r.a.} ndiye aliyezusha swala ya tarawehe,ni kauli ya urongo inayoenezwa na mashia ili kumtuhumu Sayyid'na Umar{r.a.}.

-Tarawehe ni sunna ya Mtume{s.a.w.} kwa ushahidi wa hadithi tuliyoitaja,na ama kuwa Mtume{s.a.w.} aliiwacha kuiswali kwa jamaa msikitini,hilo ni kwasababu ya kizuizi kilichojitokeza,nacho nikuogopea kushuka wah’yi ukafaradhisha swala ya tarawehe,halafu isije ikawashinda watu.

-Kizuizi hicho kiliondoka baada ya kufariki Bwana Mtume{s.a.w.},kwasababu wah’yi umekatika kwa kufa yeye,kwahiyo kule kufaradhishwa alikokuogopea Mtume{s.a.w.} hakuko tena,ndiyo Umar{r.a.} katika utawala wake akaihuisha swala hii tena, kwa jamaa msikitini.

2-Bila shaka Sayyidna Umar{r.a.} ni katika makhalifa waongofu wa Bwana

Mtume{s.a.w.} ambao tumeamrishwa tushikamane na sunna zao,kwa hiyo hata tukisema kwamba alieianzisha ni Umar,bado ni sunna kwa amri ya Mtume {s.a.w.} na mafundisho yake,au nyinyi ni mashia?

Hamuutambui ukhalifa wa Umar?na hamumtambui kwamba yeye ni khalifa mwema wa bwana mtume{s.a.w.?

3-Labda jambo litakalo kutatiza wewe,ni kauli ya Umar{r.a.},aliposema ;
"نعمت البدعة هذه" [bora ya uzushi ni huu].

Kwa ufupi ni kwamba uzushi uliokusudiwa hapa ni kwa maana ya kilugha,na siyo kisheria,kwasababu uzushi kilugha ni kila jambo jipya,na hili lilikuwa ni jambo jipya kwa watu wengi hasa wale

ambao hawakumdiriki Bwana Mtume{s.a.w.}.

Amesema Sheikhul Islami ibin Taymiyyah{r.a.t.};

“Na zaidi ya hayo ni kuiitaUmar -swala ya tarawehe-kuwa ni bidaa,pamoja na uzuri wake,na huo ni mwito wa kilugha tu,na siyo kisheria”.
tazama Iqtidhaus swiratil mustaqim uk 276

Na amesema Al hafidh ibin Kathir{r.a.t.};
“Bidaa iko sehemu mbili,mara inakuwa bidaa kisheria,kama kauli yake{s.a.w.};

[kila lenye kuzushwa ni bidaa,na kila bidaa ni upotevu”.

ama mara nyingine inakuwa bidaa ina maana ya kilugha,kama kauli ya Amiril muumina Umar bin Al khatab alipowakusanya kwenye swala ya tarewehe na wakaendelea;“bora ya uzshi ni huu”].

tazama tasfirul Qur'anil adhim 1/166.

## Hoja yao ya tatu;

Zama za Mtume{s.a.w.} hakukua na msahafu kama huu tulio nao leo,bali walioukusanya ni maswahaba kina Abu bakar,Umar,Zaid,na baadaye Uth'man,na hilo ni baada ya kufariki Mtume{s.a.w.}, kwahiyo hamuoni kwamba hiyo ni bidaa nzuri?

## Jawabu yetu ni kwa njia tatu;

1-Qur'an iliitwa kitabu tangu zama za Mtume{s.a.w.} kuishiria kwamba Qur'an itakuwa kwenye kitabu,kama ilivyo kuja

katika aya nyingi za Qur’an,miongoni mwa hizo ni ile isemayo;[hicho ni kitabu, hakina shaka ndani yake] aya ya2,sura ya 2.

2-Jambo lolote lile ambalo ameliwacha mtume {s.a.w.}kwa sababu ya kupatikana vizuizi,kisha vizuizi hivyo vikaondoka baada ya kufa kwake,
kulifanya jambo hilo baada ya kuondoka vizuizi hivyo siyo bidaa,kama kuikusanya Qur'an katika msahafu mmoja.

Na Mtume{s.a.w.} hakuweza kuikusanya Qur’an katika msahafu mmoja,kwasababu Qur’an bado inaendelea kuteremka,na Mwenyezi mungu{s.w.t.} anazibadilisha aya kama anavyotaka,na kuzifuta,kama ilivyothibiti kwamba suratul al ah’zab(33) yenye aya 73,ilikuwa kama suratul baqarah(2) yenye aya 286.

3-Kazi hii ya kuikusanya Qur’an,imefanywa na Makhalifa wema wa Bwana Mtume{s.a.w.} ambao

tumeamrishwa tushikamane na sunna zao,na miongoni mwa sunna zao njema ni huku kuisanya Qur’an tukufu,
hivyo basi siyo katika in’safu kuifananiza sunna njema iliyofanywa na Mabwana wakubwa hawa na uzushi uliozushwa na Mashia Baatiniyya wenye historia chafu dhidi ya uislamu,tena baada ya zile kar'ne tatu alizozisifia Bwana Mtume{s.a.w.} kwa ubora.

**Tafadhali fuatilia mfululizo wa jawabu za hoja zilizobakia katika makala namba 3.**

**وصلى الله وسلم وبارك على سيدنا محمد وعلى آله وصحبه أجمعين,**
**والحمد لله رب العا لمين.**